

## **KITENGO CHA KUMBUKUMBU**

### **UTANGULIZI**

Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya ina Masjala ya wazi moja na Mtunza Kumbukumbu mmoja anayehudumia watumishi wa Idara ya Afya 312, pamoja na hayo ni kwa ajili ya kuandaa farihisi (Index) na nyenzo nyingine za kurahisisha upatikanaji wa nyaraka kwa urahisi, pia kupokea na kushughulikia maombi mbalimbali ya watumishi wa Idara ya Afya yaliyoelekezwa kwa Mkurugenzi Mtendaji (W) na maafisa wengine kwa ajili ya utekelezaji wa haraka.

### **MAFANIKIO**

- Upatikanaji wa nyaraka wa watumishi na zisizo za watumishi kwa haraka.
- Kuwepo kwa kiwango kikubwa cha usiri katika upokeaji na utunzaji wa kumbukumbu katika Ofisi ya Mganga Mkuu wa Wilaya.
- Huduma bora kwa wateja (Customer Care)
- Ushirikishwaji mzuri kutoka kwa Mkuu wa Idara na Maafisa wengine.

### **CHANGAMOTO**

- Kutokuwepo kwa mfumo wa Kielektroniki katika chumba cha kutunzia kumbukumbu ili kuendana na Teknolojia ya kisasa.

### **MIKAKATI**

- Kuboresha chumba cha kutunzia kumbukumbu zilizotumika na zinazo endelea.
- Kuelimisha watumishi juu ya umuhimu wa utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali.
- Kutokuwepo na mwingiliano katika chumba cha kutunzia kumbukumbu.